

HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU

(Barua zote za Kiofisi zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Mkoa wa Arusha
Telegram: Meru
Simu: (+ 255) 027 254-1112
Faksi: (+ 255) 027 254-1112
Barua pepe:ded@merudc.go.tz
Unapojibu tafadhali taja:



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
P.O. Box 462,
USA – RIVER
ARUSHA

Kumb. Na. S.20/86/40

19/12/2017

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa ya kuomba nafasi ya Ajira ya Watendaji wa Vijiji kwa masharti ya Kudumu tangazo hili ni baada ya kupokea kibali cha ajira mbadala chenye Kumb. Na. FA 170/371/01/71 cha tarehe 08.11.2017 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mchanganuo wa nafasi hiyo ni kama ifuatavyo:-

1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III - Nafasi 20

(a) KAZI NA MAJUKUMU

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- ii. Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
- iii. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- iv. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
- v. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa Kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- vi. Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalmu katika Kijiji
- vii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji
- viii. Mwenyekiti wa kikao cha wataalamu waliopo katika Kijiji
- ix. Kupokea kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi
- x. Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji
- xi. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

(b)SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe na cheti cha kidato cha nne/ sita.
2. Awe na cheti (Astashahada) kati ya moja ya fani zifuatazo:- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya jamii na Sayansi ya sana toka chuo cha Serikali za mitaa Hombolo au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

(c)NGAZI YA MSHAHARA

TGS. B1 yaani 390,000/= kwa mwezi.

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE AMBAO NI LAZIMA KUZINGATIA

1. Mwombaji ni lazima awe raia wa Tanzania
2. Awe hajawahi kufungwa kwa makosa ya Jinai
3. Awe hajawahi kufukuzwa au kupunguzwa kazi Serikalini
4. Maombi ni lazima yaambatanishwe na vivuli vya vyeti vya Kuzaliwa, Kuhitimu Elimu ya Sekondari (Results Slip – Hazikubaliki) na vyuo vya mafunzo au Taaluma
5. Maombi ni lazima yaambatanishwe na picha mbili za "passport size" za hivi karibuni
6. Maombi ni lazima yaambatanishwe na wasifu "Curriculum Vitae" zenye mawasiliano ya uhakika, Anuani, Barua pepe na namba za simu
7. Awe na Umri wa zaidi ya miaka 18 na usiozidi miaka 45
8. Mwombaji awe hajawahi kuajiriwa Serikalini na kupata check Namba
9. Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne na cheti cha taaluma ambavyo vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA) na Baraza la Elimu ya Ufundi wa Taifa (NACTE)

Mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe **03/01/2018** saa 9.30 Alasiri. Pia maombi yote yatumwe kwa anwani zifuatazo.

**Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Meru,
S. L. P 462
USA - RIVER**

Tangazo hili pia linapatikana kwenye Tovuti ya Halmashauri www.merudc.go.tz na mbao za matangazo.

Tangazo hili limetolewa na:



Grace Mbilinyi

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU**

